



22120298



International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

SWAHILI A1 – HIGHER LEVEL – PAPER 2
SWAHILI A1 – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 2
SWAHILI A1 – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 2

Tuesday 15 May 2012 (morning)

Mardi 15 mai 2012 (matin)

Martes 15 de mayo de 2012 (mañana)

2 hours / 2 heures / 2 horas

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question only. You must base your answer on at least two of the Part 3 works you have studied. You may include in your answer a discussion of a Part 2 work of the same genre if relevant. Answers which are not based on a discussion of at least two Part 3 works will not score high marks.
- You are not permitted to bring copies of the works you have studied into the examination room.
- The maximum mark for this examination paper is *[25 marks]*.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Traitez un seul sujet de composition. Vous devez baser votre réponse sur au moins deux des œuvres de la 3^e partie que vous avez étudiées. Le cas échéant, vous pouvez inclure dans votre réponse une discussion sur une œuvre du même genre littéraire étudiée dans la 2^e partie du programme. Les réponses qui ne sont pas basées sur au moins deux des œuvres de la 3^e partie n'obtiendront pas une note élevée.
- Vous n'êtes pas autorisé(e) à amener des exemplaires des œuvres que vous avez étudiées dans la salle d'examen.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d'examen est *[25 points]*.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Elija un tema de redacción. Su respuesta deberá basarse en al menos dos de las obras estudiadas en la Parte 3. Se podrán hacer comentarios sobre una obra de la Parte 2 del mismo género, si fuera necesario. Las respuestas que no incluyan una discusión sobre al menos dos obras de la Parte 3 no recibirán notas altas.
- No se permite traer a la sala de examen copias de las obras estudiadas.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es *[25 puntos]*.

Jibu swali moja tu la insha. Jibu lako liegemee kwenye angalau kazi mbili za kazi za sehemu ya 3 ulizojifunza. Unaweza kuingiza katika jibu lako majadiliano ya kazi ya sehemu ya 2 ya utanzu huohuo ambao umejitayarisha nao. Majibu ambayo hayana mjadala wa angalau kazi mbili za sehemu ya 3 hayatapewa alama nyingi.

Tamthilia

1. Onyesha maudhui yanayojadiliwa katika kazi za waandishi wawili tofauti ulizojitayarishia na uonyeshe vile wanavyotumia mbinu tofauti katika kufanikisha maudhui haya.
2. Fasihi huwa kama jua linalochomoza na kuwaletea wateja wake mwanga lakini linapotua, hulete kiza na kumnyima binadamu nafasi ya kuona mbali. Jadili kauli hii ukizingatia kazi mbili kutoka kwa waandishi wawili tofauti ulizosisoma.

Riwaya

3. Onyesha vile dhana ya jazanda na istiara inavyokuzwa na waandishi wawili wa kazi mbili tofauti ulizosisoma na ujadili jinsi mbinu hizi zinavyofanikisha kazi zao.
4. Kazi za riwaya huathiriwa sana na mitazamo na mazingira wanamokulia. Onyesha vile mitazamo hii inavyoathiri kazi za fasihi katika kazi mbili tofauti kutoka kwa waandishi wawili tofauti ulizojitayarishia.

Ushairi

5. Huku ukizingatia kazi za wanashairi wawili ulizojitayarishia, jadili ni kwa kiwango kipi na kwa njia zipi waandishi hawa wanavyojaribu kuwasawazishia wasomi wao kwa kutumia lugha na mbinu zinazoeleweka.
6. Linganisha uteuzi wa mada kama ulivyotekelezwa na waandishi wa kazi mbili tofauti ulizosisoma na ujadili vile wanavyoshabihiana au kutofautiana katika kutekeleza swala hili.

Riwaya za mapenzi

7. Waandishi tofauti hutumia mifumo na mitindo tofauti katika kukuza swala la mapenzi. Onyesha vile waandishi wawili wa kazi mbili ulizozisoma wanavyotekeleza swala hili.
8. Lugha inayotumika kwenye riwaya za mapenzi inashabihiana kutoka kwa mwandishi mmoja hadi mwingine. Onyesha vile waandishi wa kazi mbili tofauti ulizozisoma wanavyotumia vipawa vyao vya ubunifu kwa kudhihirisha au kukanusha msemo huu.

Maswala ya ujumla

9. Onyesha nyezo za fasihi zinazotumiwa katika kukuza vipawa tofauti na ujadili jinsi waandishi wawili wa kazi mbili tofauti ulizojitayarishia wanavyofaulu au kutofaulu katika kutekeleza jambo hili.
 10. Ingawa fasihi kazi yake ni kuliwaza na kuzindua wasomi, mara nyingi huwapumbaza na kuwapa sera zisizokuwa na misingi. Jadili kauli hii ukizingatia kazi mbili kutoka kwa wasanii wawili tofauti ulizojitayarishia.
 11. Je, fasihi hufunza uadilifu katika jamii? Jadili huku ukionyesha waandishi wawili wa kazi ulizozisoma walivyotekeleza jukumu hili.
 12. Uandishi ni njia moja ya kuendeleza mawazo tofauti ya waandishi. Onyesha jinsi waandishi tofauti wanavyotumia ploti tofauti kutekeleza mawazo haya.
-